

## *SURA YA KWANZA*

Asubuhi yenye kupendeza Gloria binti mzuri alikuwa chumbani kwake akijiandaa kuelekea katika chumba cha Darasa alikuwa ni binti mwenye rangi ya weusi wenye kuteleza akiwa anajiangalia kwenye kioo nakunyoosha nguo zake simu yake ya mkononi inaita.

“Nani ananipigia asubuhi yote hii?” anajiuliza nakushindwa kuipokea.

“siwezi kuipokea namba siijui” anapuuzia nakuendelea nakazi alikuwa si mtu mwenye maringo alikuwa mtu makusikiliza nakujali wengine,

kitandani kulikuwa na Bahasha ndogo iliyokuwa na ujumbe ndani pamoja na uwa zuri lililokuwa na mchoro wenye alama ya kopa na rangi nyekundu.

“Nilipewa na rafiki yangu huwo mzigo kaniambia umetoka kwa moja ya wahadhiri hapa chuoni!” anaingiwa na hali ya mshangao kila mala anapoangalia ile bahasha nakuona alama ile ya kopa akimfikiria mhadhiri huyo aliyoituma Bahasha hiyo.

“Mbona mhadhiri ni mtu mzima na msomi anawezaje kunitumia...kama hii?” anajiuliza Gloria huku akiwa anavaa nguo zake nywere zake zilikuwa nzuri nazenye kuteleza kila anapotaka kuisoma nikama anajuwa kile kitakachokuwa kimeandikwa ndani,

“Hakuna kitu kingine zaidi ya ujumbe wakimahusiano” anasogea kitandani nakuiangalia Bahasha hiyo “Mmmh” anaguna Gloria huku akiwa anasikitika “nashindwa kuelewa kwanini inakuwa hivi kwa mtu mzima na msomi kama yule” anamfikiria mhadhiri huyo.

Kipindi alichokuwa akienda kuingia ilikuwa nicha mhadhiri huyo aliyeituma Bahasha hiyo yenye ujumbe wenye maneno mazuri ya hisia za mapenzi,

Gloria anaondoka chumbani kwake akiwa amebaba begi lake dogo lililokuwa na kompyuta mpakato alikuwa binti aliyekuwa akivaa nguo za heshima na mwenye utulivu "Gloria nisubiri" anasema binti ambae walikuwa wanaishi nae pamoja.

"Tumechelewa" anasema Gloria akiwa anaangalia saa yake ya mkononi,

"kweli halafu sijui mhadhiri yule huwa anatabia yakurudisha watu nje wanao chelewa Rectural yake.

"Mmh!" anaguna huku akiwa anafikiria Gloria mala atakapo chelewa itakuwaje kwa mtu ambae ameshaanza kuonyesha hisia za mapenzi inakuwa siri yake "twende" wanaambatana nakushuka ngazi kuelekea katika Rectural,

Ulikuwa umbali wa mita chache kutoka jengo walilokuwa wakiishi hadi jengo lakutolea Rectural "ameshaingia" anasema binti aliyeishi chumba kimoja na Gloria.

"Tuingie akiturudisha basi tutarudi" anaongea Gloria akiwa anajiamini wanakubaliana nakusonga hadi chumba cha kutolea Rectural "Nye mnao ingia sasa hivi mlikuwa wapi?" anauliza akionekana kubadirisha sura yake Gloria na binti mwenzake anakaa kimya bila kujibu chochote,

"Haya naomba rudini nje kama hamna majibu" kutokana na maneno hayo Gloria anatoka nje akiwa na binti mwenzake "tufanyeje sasa?" anauliza binti mwenzake akimuuliza Gloria.

"Hatuna lakufanya" anaondoka Gloria nakuelekea pembeni mita chache na jengo la kutolea Rectural,

Muda wa saa moja unapita Rectural inaisha mhadhiri anapotoka nakumuona binti Gloria ambae hisia zake alizielekeza kwake anasimama nakumuita, "Njooi ofisini kwangu" anazungumza huku akiondoka akiwa amevaa suti mkononi akiwa ameshikilia begi lake lilokuwa na vifaa vyakufundishia.

"Mmh ametuita ofisini kwake" anasema binti mwenzake Gloria akiwa nawasiwasi akijuwa huwenda akawa anaenda kuwachukulia maamuzi magumu "sijui ngoja tukamfuate nakumsikiliza" anajibu kwa upole Gloria,

kwajinsi alivyokuwa mzuri alikuwa na mvuto kwa watu wengi utaratibu nakutokuwa na pupa ilikuwa jadi yake "ataenda kutuambia nini?" anajuliza Gloria.

Baada ya dakika chache wanaingia ofisini kwa mhadhiri huyo "hodi" anabisha hodi mwenzake na Gloria waliyekuwa wameambatana naye "ingia" anasema mhadhiri akiwa amekaa akiangalia vitu katika kompyuta mpakato.

Wanasukuma mlango nakuvingia ndani Gloria akifuata nyuma mhadhiri anapomuona anaingwa na tabasamu kisha anawauliza, "kwanini mmechelewa kuingia kwenye kipindi changu?" anawauliza huku akikaa kimya kuwasikiliza,

"samahani nihali ya ubinadamu kupitiwa" anajibu kwa upole Gloria kila alipokuwa anaongea dimpozi zake zilimvutia mhadhiri, "Dah huyu binti ni mzuri sana" anawaza akilini huku akiwa anamuangalia nakumsikiliza kwa umakini.